

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA MAGANZO (“MAGANZO WSSA”) KWA MWAKA 2017/18 – 2019/20

Maombi ya Mapendekezo ya Bei Na. TR -W-17-006

Mnamo tarehe 15 Agosti 2017 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi ya kwanza kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Maganzo (Maganzo WSSA) ya mapendekezo ya bei za magati, bei za maji kwa wateja wote wanaotegemewa kuunganishwa katika matandao wa maji, pamoja na ada mbalimbali kwa mwaka 2017/18 – 2019/20. Jedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei na ada zinazopendekezwa.

Jedwali Na 1: Bei Zinazopendekezwa za Magati (Sh./Lita 20 na Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Unitu ya ujazo)

Kundi la Wateja	2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	1,125	1,125	1,125
Taasisi	1,200	1,200	1,200
Biashara	1,350	1,350	1,350
Magati	35	35	35

Jedwali Na 2: Ada Inayopendekezwa ya Maunganisho ya Huduma ya Maji (Shilingi kwa Maunganisho

Kundi la Wateja	2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	25,000	25,000	25,000
Taasisi	25,000	25,000	25,000
Biashara	25,000	25,000	25,000

Jedwali Na 3: Ada Inayopendekezwa ya Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa huduma (Shilingi/Kurejeshewa huduma)

Kundi la Wateja	2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	6,000	6,000	6,000
Taasisi	6,000	6,000	6,000
Biashara	6,000	6,000	6,000

Jedwali Na 4: Tozo ya Huduma Inayopendekezwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	2,000	2,000	2,000
Taasisi	2,000	2,000	2,000
Biashara	2,000	2,000	2,000

Jedwali Na 5: Ada Inayopendekezwa ya Fomu Ya Maombi ya Huduma (Sh./Fomu)

Kundi la Wateja	2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	2,000	2,000	2,000
Taasisi	2,000	2,000	2,000
Biashara	2,000	2,000	2,000

Hii ni mara ya kwanza kwa Maganzo WSSA kuomba mapitio ya bei. Wasilisho la mapendekezo ya bei na ada kwa EWURA ni kuzingatia kifungu cha 28 (d) cha Sheria ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 na kifungu cha 7 (1)(b)(iv) cha Sheria ya EWURA, Sura 414. Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Ijumaa, tarehe 15 Septemba 2017 katika Ukumbi wa Maganzo BM Conference uliopo mji wa Maganzo** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Tarehe ya mwisho ya kusajili lengo la kuingilia (intervene) wasilisho ni tarehe 6 Septemba 2017. Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 15 Septemba 2017**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi ya EWURA, **GHOROFA YA SABA, LAPF PENSIONS FUND TOWER; MKABALA NA KIJJI CHA MAKUMBUSHO, KIJITONYAMA, DAR ES SALAAM** au ofisi za Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Maganzo.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

31 Agosti 2017